

COMPANY HIGHLIGHT

# Tafakuri ya Menejimenti ya KVTC

na Irene Mathew & Arlene Gomes

## Tafakuri

KVTC iliandaa tafakuri kwa timu ya menejimenti ya ngazi za juu kuanzia Februari 22 – 24. Tafakuri hiyo iliwezeshwa na taasisi ya Empower Limited. Kwa menejimenti wa KVTC hii ilikuwa mara ya kwanza kwenda nje ya bonde la kilombero kama timu na kutumia akili yote kufikiria kimkakati juu ya biashara yetu. Ilikuwa ni uzoefu tofauti na mafunzo ya kawaida au kongamono/warsha kwa kawaida tunazozifanya.

KVTC inaamini kuwekeza katika mtaji wa binadamu ni lazima kwa kampuni kuendelea kwenye nyanja za biashara. Mwezeshaji Miranda Naiman alileta uzoefu mkubwa katika kuijenga timu na mpango wa kimkakati na matokeo yake tuliweza kutumia mawazo mapya na dhana za biashara katika biashara yetu ya kawaida ya misitu. Ingawa tafakuri ilikuwa ya kutopumzika haikutuchosha.

## Kutoka Nje

Manufaa ya kutoka nje ya ukanda wa mazoea na kujitenga katika eneo la pembezoni fukwe za burudani tuliweza kuwasiliana kati yetu katika timu nje ya ratiba ya kila siku ya usimamizi. Tulijifunza mengi kati yetu kuhusu wasifu binafsi na historia na matokeo tuliweza kutafakari njia bora zaidi ya kukamilisha vitu kama timu.

Kulikuwa na vichekesho, tulijifunza juu ya umuhimu wa kufanya kazi kama timu na kutengeneza mwelekeo mzuri kulingana na malengo ya kampuni na misukumo ya kibiashara. Tulikuwa na uelewa mzuri wa kila mmoja wetu kuhusu nguvu na udhaifu na namna gani ya kupata usaidizi kutoka kwa kila mmoja wetu katika shughuli za kila siku.

## Kwenda Mbele

Mwisho wa siku ya tatu ulifikia kwenye pointi tunatakiwa kurudi kwenye vituo mbali mbali vya kazi, office, kiwanda na mashambani kurejesha mawazo katika utekelezaji. Timu ya menejimenti ina malengo ya wazi yaliyo andaliwa kwa mwaka mzima. Mmoja ya lengo ni kuvutia wengine katika timu ya KVTC katika kile tunachopenda nini muonekano wa KVTC mwisho 2019 na miaka mingi ya baadae.

Washiriki wote wa Tafakuri watapimwa kulingana na malengo yaliyokubaliwa na walichofanikiwa kutekeleza.

## Empower

Tafakuri iliwezeshwa na Empower Ltd. Empower ni Taasisi ya Ushauri ya Mtaji wa Raslimali watu inayojishughulisha na uajiri na program ya mafunzo kulingana na mahitaji ya mteja.

HIGHLIGHTS



## Mradi wa P4F, MCDI & KVTC

Mwezi Machi mradi mpya wa ubia wa ushirikiano kwa ajiri ya Misitu (P4F), Jitihada ya Maendeleo ya Uhifadhi wa Miombo (MCDI) na KVTC umeanza.

P4F na MCDI zitaisadia KVTC kuboresha usimamimizi wa ardhi ya misitu ya asili na kutafuta njia mpya ya kutengeneza shughuli zitakazo zalisha kipato kwa jamii inayotuzunguka. Wakati huohuo KVTC itaisaidia MCDI katika uendelelezaji wa shughuli za kibiashara kwa vijiji vilivyo chini ya msaada wao.

P4F ni program inayofadhiliwa na kitengo cha Uingereza kwa ushirikiano wa mataifa na kitengo cha biashara, nishati na mkakati wa viwanda (BEIS) kinachofanya kazi Africa, Asia na Latin America. P4F kina lenga kupunguza kutoweka kwa misitu kwa kuchochea uwekezaji endelevu wa misitu na matumizi bora ya ardhi. Kuvutia uwekezaji wa P4F inaangazia ubia unaotoa manufaa ya pamoja yenye mvuto kwa sekta binafsi, sekta ya umma na wabia wa umma.

MCDI ina himiza uhifadhi wa misitu ya asili Kusini Mashariki ya Tanzania kwa kutafuta na kutengeneza fursa kwa jamii husika kuweza kunufaika kutokana na usimamizi endelevu wa misitu yao.

# Kutoka Dawati Hans

na Hans Lemm

Mvua zimeendelea kuwa za kusua sua wakati tunaelekea kumaliza msimu wa upandaji, tungependa kuona ukuaji wa kasi wa upandaji mpya lakini tusubiri matumaini ya miezi miwili ya msimu litaleta mshangao wa mabadiliko chanya.

Kwa upande wa swala chanya timu ya uongozi wa ngazi ya juu KVTC walipata fursa ya kutumia siku tatu nje ya ratiba ya kila siku na kufikiri kimkakati zaidi kuhusiana na muelekeo wa biashara na vilevile kuja pamoja kama timu. Irene na Arlene watashirikisha uzoefu wao katika Makala ijayo.

Mwezi Machi mimi na CEO mpya KVTC tulipata fursa ya kutembelea wateja muhimu. Irvine anatushirikisha mtazamo wake juu ya ziara katika hili jarida.

Kama ilivyo vitu vyote vizuri vinafikia mwisho, sawa na utendaji wangu KVTC. Ilikuwa ni heshima kuongoza kampuni hii kwa miaka kadhaa na nimeridhika na mafanikio yake.

Ningependa kuwashukuru wafanyakazi wetu, wateja, wawekezaji na wadau wote wengine kwa msaada mlio nipa na kampuni kwa miaka 11 iliyopita na uhakika mtaendelea kuiunga mkono KVTC na kuiweka katika kiwango cha juu zaidi.

Ningeppeenda kuchukua fursa hii kumtakia mrithi wangu mafanikio yote katika jukumu lake jipya na lenye changamoto na kuelezea imani yangu uongozi mpya na mawazo mapya ni vitu vizuri kwa KVTC na kampuni itanufaika kutokana na badiliko hili.





March '19: KVTC Team visiting customers in New Delhi; KVTC Teak in the background

# Ziara ya India: Soko Kuu la KVTC

na Irvine Kanyemba

## India

India ina idadi ya watu bilioni 1.4 kuifanya nchi yenye demokrasia kubwa kabisa ulimwenguni. Ni nchi yenye historia ya mvuto na tajiri wa tamaduni. Africa kwa upande mwingine ina idadi kubwa ya wahindi nje ya bara hindi.

Wahindi wanajulikana duniana kwa kuwa na maadili imara ya kazi na ujuzi wa biashara. Na hii inajionyesha kwenye biashara ya mbao za mtiki na sekta ya uchakataji India. Sekta imetawaliwa kwa uwiano na kaya ndogo zinazo milki kampuni. Ingawa hawatumii vifaa vya kisasa, kwa ujumla wanaviendesha kwa ufanisi na vinatoa faida.

## Mtiki ni Mbao

India ina ingiza 75% ya mitiki inayozalishwa ulimwenguni. Ina nunua kiasi cha 100,000 $m^3$ ya mbao za mitiki (magogo na mbao zilizo chanwa) kwa mwezi. Hii inatumika zaidi kutengeneza milango, flemu za milango, madirisha, maumbo na thamani. India, Mtiki ni mbao ya chaguo na inapewa thamani kubwa kwenye soko.

Kuna kitu kinajitokeza kwenye hili soko ni uingizaji India wa bidhaa zilizofanyiwa kazi kwa kiasi kutoka, mara nyingi, viwanda vinavyosimamiwa na Wahindi vilivyopo Africa, Kusini na America ya Kati. KVTC ni kiongozi katika mwelekeo huu, kwa kutoa sehemu ya magogo kwa viwanda na kuwakaribisha watumiaji wa mwisho wengi kujenga viwanda vya kukata kulingana na wateja karibu na eneo la gogo za KVTC.

## Mwelekeo wa Masoko

Kwa sasa, mahitaji ya Mtiki India kwa ujumla kuna changamoto hususani kwa saizi ndogo na mbao (size board) zina pata ushindani mkubwa kutoka kwa nchi zinazosafirisha kama Ecuador na Ghana. Mahitaji kwa saizi kubwa bado ni imara.

KVTC imeitikia kwa kufanya kazi katika sehemu tofauti tofauti za soko na kijiografia India. Uwezo wa kubadilika ndio moja ya nguvu ya KVTC na wakati hali ya ushindani wa soko ni changamoto kwa KVTC ambayo imejiweka vizuri tayari kulishughulikia.

Mtazamo wa soko ni kwamba mahitaji yataongezeka baada ya uchaguzi mkuu utakao fanyika India kutoka Aprili mpaka Mei mwaka huu.

### WORKING GROUP MSITU

KVTC imefurahi kuwa mwanachama kwenye Working Group Msitu (FWG) kinacho fanya kazi chini ya Baraza la Taifa la Biashara Tanzania).

Mwezi January mkutano wa kwanza ulifanyika, na tumevutiwa kwa kuweza kusaidia kuchangia mtazamo wa mbele misitu Tanzania.

### TUSIKILIZE

**Sikiliza Kipindi cha Mitiki Yetu**

Kwenye Radio Pambazuko 89.5FM

Kila Ijumaa 01.30 jioni na kila Jumamosi 01.30 asubuhi

### WASILIANA NASI

WASILIANA NASI AU TUANGALIE :
kvtc@kvtc-tz.com / http://kvtc-tz.com/

PO Box 655, Ifakara, TZ

PO Box 12452, Dar es Salaam, TZ